

# HALMASHAURI YA WILAYA YA KWIMBA



Kumb. Na. Kumb. Na. MZA/KDC/M.70/35

Tarehe 15/01/2018

## **TANGAZO LA KUPATA MAFUNDI KATIKA KITUO CHA AFYA MALYA.**

Kwa kuzingatia maelekezo ya Serikali ya Jamhuri wa Muungano wa Tanzania ilivyoagiza kutumia mafundi wa kawaida katika miradi mbalimbali ya ujenzi wa majengo ya Serkali. Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kwimba anapenda kuwakaribisha mafundi **uashi( mansory,wenye uwezo wa kujenga kwa kutumia tofali za hydraform, saruji) ,Fundi seremala,(carpentry),Fundi umeme,(electrical),bomba (Plumber) na Fundi wa kazi za umaliziaji kwa mfano lipu, Kupaka rangi, .n.k** kwa ajili ya kufanya kazi za ujenzi wa:-

- i. Jengo la kuhifadhia maiti(Mortuary)
- ii. Jengo la Wazazi (ward)
- iii. Jengo la Maabara
- iv. Jengo la upasuai na
- v. Nyumba ya mtumishi

### **1. SIFA za mwoombaji ni lazima:-**

- i. Awe ni mkazi katika wilaya ya Kwimba na raia wa Tanzania
- ii. Awe anajua kusoma Ramani na Michoro
- iii. Awe anajua kusoma na kuandika kwa Kiswahili au kiingereza
- iv. Awe na uzoefu wa kazi usiopungua miaka mitatu (3) katika ufundi wake
- v. Mwombaji awe na umri wa miaka 18 na kuendelea na awe mwaminifu.
- vi. Awe tayari kutekeleza kazi zote zinazohusiana na ujenzi atakazopangiwa na msimamizi wake wa kazi

- vii. Mwombaji ni lazima athibitisha kazi za Ujenzi alizokwishafanya kwa kutaja maeneo aliyowahi kufanya kazi kama aliyoomba kwa kuambatisha picha za kazi hizo.
- viii. Mwombaji asiwe na kazi nyingine anayoendelea nayo.

## **2. JINSI YA KUTUMA MAOMBI**

Mwombaji ni lazima aandike barua ya kuomba kuwasilisha vigezo vyake vya ufundi na kuikabidhi **Ofisi ya Kitengo cha manunuzi na Ugavi (W) au Ofisi ya Mtendaji wa Kata ya Malya** ikiwa imefungwa vizuri kwenye bahasha na juu iandikwe anwani ifuatayo;-

Mkurugenzi Mtendaji(W), Halmashauri ya Wilaya ya Kwimba, S.L.P 88, Ngudu/Kwimba.

## **3. MWISHO WA KUPOKEA BARUA ZA MAOMBI**


- Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 18/01/2018 saa 9:30 alasiri

## **4. USAILI**

- Usaili utafanyika siku ya ijumaa tarehe 19/01/2018 kuanzia saa 4:00 asubuhi katika Kituo cha Afya Malya.

**NB;**

- **MAFUNDI WATAKAOPEWA KIPAUMBELE NI WAKAZI WA WILAYA YA KWIMBA HASA KATA YA MALYA.**
- **MICHORO YA MAJENGO ITATOLEWA KWA MAFUNDI WATAKAOFAULU USAILI SEHEMU YA KWANZA ILI WASOME NA WAJAZE BEI ZAO ZA UJENZI KWA AJILI YA KUSHINDANISHWA KWA AWAMU YA PILI.**



Stamili A. Ndaru

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji (W)  
Halmashauri ya Wilaya ya Kwimba,